

MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF) HANDENI

Nini maana ya mfuko wa afya ya jamii?

Ni mpango wa kisheria wa bima ya Afya ambapo mwananchi anawajibika kuchangia huduma za afya kabla ya kuugua. CHF ilianzishwa chini ya sheria Na 21 ya mwaka 2001. Wilaya ya Handeni ilianza baada ya kupatikana sheria ndogo iliyotangazwa kwa tangazo la Serikali Na.288 tarehe 16/9/2005.

JE, Ni kiasi gani kinachochangiwa kwenye CHF?

Kiwango kinachochangiwa hutofautiana kati ya Halmashauri moja na nyingine. Kwa Handeni kiwango cha kuchangia ni Tsh.20000/= kwa mwaka mzima.

JE, Tele kwa tele ni nini?

Ni mchango wa serikali kwa kila kaya iliyotoa mchango wa CHF kwa mwaka. kiasi kilichotolewa na Serikali ni sawa na kile ambacho mwananchi amechangia. Kwa Halmashauri ambazo kiwango cha kuchangia ni kikubwa hunufaika kwa kupata fedha nyingi kutoka Serikalini na kwa wale wanaochangia kiwango kidogo hupata fedha kidogo.

JE, Ni nini tafsiri ya Kaya?.

Kaya inaundwa na watu wasiozidi 6. Aina za kaya kwa mujibu wa CHF ni.

1. Baba, mama na watoto chini ya umri wa miaka 18; AU
2. Mtu mmoja au zaidi mwenye umri zaidi ya miaka 18 mfano vikundi vya uzalishaji mali , VICOBA;AU
3. Taasisi, mfano shule (wanafunzi).nk

JE, wapi waweza kujiunga na CHF

Unaweza kujiandikisha kwenye kituo chochote kinachotoa huduma kwa wanachama wa CHF ambapo mwanachama anategemea kupata huduma.

JE, Ni huduma gani zitolewazo kwa mwanachama wa CHF?

- Usajiri dirishani.
- Kumwona daktari.
- Huduma za maabara (vipimo).
- Dawa bure.
- Upasuaji mdogo.
- Kulazwa
- X-Ray
- Kitambulisho

JE, Kuna faida gani kujiunga na CHF.

1. Kunufaika na mchango wa Serikali wa tele kwa tele.
2. Kuokoa fedha za matibabu ambazo zingeweza kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo.
3. Mwanachama anakuwa na uhakika wa kupata huduma bora wakati wowote kwasababu mchango wake unawezesha kituo cha huduma kununua dawa /vifaa kabla mwanachama hajaagua.
4. Kupunguza msongo wa mawazo ndani ya familia endapo utaugua au kuuguliwa.